# Ufundishaji wa Kusoma na Kuandika Kiswahili: Uzoefu wa Idara ya Lugha na Taaluma za Kiafrika, Chuo Kikuu cha Sebha, Libya

*Idriss Hassan Elmahdi*

*Ikisiri*

Makala haya yanahusu shughuli za kufundisha Kiswahili kama lugha ya kigeni katika Chuo Kikuu cha Sebha nchini Libya. Kwanza inaeleza historia ya Kiswahili – yaani kilianza lini kufundishwa kwa madhumuni gani na nani walikuwa wanzilishi. Halikadhalika makala ya naeleza utaratibu uliowekwa na idara ili kuweza kufundisha stadi hizi kama sehemu ya kumfundisha mwanafunzi kuandika kwa hati ya Kirumi na wakati huohuo kumsaidia kuimarisha ujuzi wake wa Kiswahili. Matatizo na mbinu za kuyatatua na mafanikio yaliyopatikana yanaelezwa pamoja na mustakabali uliopo wa Kiswahili katika Idara ya Lugha na Taaluma za Kiafrika, Chuo Kikuu cha Sebha nchini Libya.

## 1.0 Utangulizi

Kufuatia Mapinduzi ya Septemba 1969, pamekuwa na msukumo wa kupata ukombozi wa Bara la Afrika kutoka kwa Wakoloni ambao waliiba hazina zake bila gharama yoyote na kukandamiza utambulisho wa fahari na utamaduni wa pekee wa Waafrika. Hii ni pamoja na kufutilia mbali lugha za Kiafrika na badala yake kuweka lugha zao za Kizungu katika bara hili adhimu duniani. Ili kurudisha utukufu na fahari yake iliyopotea, idara ya Kiswahili ilianzishwa Chuo Kikuu cha Sebha nchini Libya chini ya Kitivo cha Sanaa mnamo mwaka 1984 /1985. Idara ilianza ikiwa na walimu wageni watatu waliotoka nchi mbalimbali za Afrika. Idara hii tangu ilipoanza kufundisha mpaka leo (mwaka 2011), imehitimisha awamu za wanafunzi. Miongoni mwa wanafunzi wa awamu hizo tayari wanafanya kazi katika sehemu mbalimbali za utumishi wa umma kama vile katika Kamati Kuu ya Mambo ya Nje, Idara Kuu ya Uhamiaji, na Kamati Kuu ya Elimu na Sayansi.

Vilevile idara ya Kiswahili imejengwa na mikono ya wanafunzi wake ambao walihitimu masomo yao na wakapata Shahada ya kwanza ya Kiswahili hapa Nchini Libya katika Chuo Kikuu cha Sebha, katika Idara ya Lugha na Taaluma za Kiafrika. Baadhi yao waiamua kuendelea katika masomo yao ya juu mpaka wakapata Shahada ya Juu na baadaye Shahada ya Udaktari nchini Tanzania. Sasa wamesharudi nchini ili Kufundisha Kiswahili katika Idara ya Lugha na Taaluma za Kiafrika, Kitivo cha Sanaa, Chuo Kikuu cha Sebha. Idara ya Lugha na Taaluma za Kiafrika nchini Libya ilikuwa ni idara ya kwanza kufunguliwa katika sehemu ya Afrika ya Kaskazini na Nchi za Kiarabu mnamo mwaka 1984. Tunamshukuru Mwenyezi Mungu kuhusu maendeleo ya Kiswahili yalivyo sasa nchini Libya. Kabla ya Mwaka 1984/1985 kulikuwa na Walibya wachache sana

waliojua Kiswahili. Lakini leo kuna idadi kubwa ya watu wanaofahamu Kiswahili siyo wanajua tu. Kiswahili sasa nchini Libya kinafundishwa katika shule za awali, shule za sekondari na baadhi ya vyuo vikuu. Kiswahili sasa ni lugha maarufu sana nchini Libya.

## 2.0 Umuhimu wa Stadi za Kusoma na Kuandika katika Kujifunza Lugha

Umuhimu wa stadi za kusoma na kuandika katika kujifunza lugha ni kumpa mtu anayejifunza lugha uwezo wa kusoma na kuandika lugha hiyo. Katika ulimwengu wa sasa, haitoshi mtu kujua tu kuzungumza lugha. Ili aweze kuwasiliana na watu wengi zaidi wanaoijua lugha hiyo, na hasa wale wanaoishi mbali naye, inambidi mtu huyo ajue kuiandika au kuisoma lugha hiyo. Kujua kusoma na kuandika ni ufunguo wa milango ya mawasiliano na elimu. Kwa kujua kuandika ataweza kuwapelekea habari wanaoishi mbali naye na kwa kujua kuisoma ataweza kupata habari kutoka kwa watu hao. Si hivyo tu bali pia, kujua kusoma na kuandika lugha kunamwezesha mtu kusoma kumbukumbuku mbalimbali za matukio yaliyopita, makubwa na madogo, yake binafsi au ya jamii yake, ambayo kwa pamoja yanajenga historia ya jamii au nchi kwa vizazi vya sasa na vizazi vijavyo. Isitoshe, hazina kubwa ya maarifa na elimu mbalimbali iliyo katika maandishi haitakuwa yenye faida kwa mtu asiyeweza kusoma kilichoandikwa. Halikadhalika ili naye aweze kutoa mchango wa maarifa au elimu inambidi ajue kuandika ili watu wengine waweze kunufaika kwa mchango wake atakaotoa.

Lakini tunapaswa kuelewa kuwa Kusoma na Kuandika kulikotimia ni kule kunakomwezesha mtu kusoma au kuandika kwa ufasaha na kueleweka bila matatizo na watu wengine wanaomsikia au wanaosoma maandishi yake. Lengo hilo haliwezi kufikiwa kwa siku moja au siku chache na mwanafunzi anayejifunza lugha. Ni kazi inayohitaji kujengwa kupitia hatua nyingi zilizopangwa kwa utaratibu mzuri na inayohitaji pia muda wa kutosha. Kwa kutambua hivyo, idara yetu imepanga kozi za kusoma na kuandika kwa mihula yenye mada mbalimbali ili hatimaye mwanafunzi anapohitimu aweze kusoma na kuandika kwa kiwango ambacho kitamwezesha kuwa msomaji na mwandikaji mzuri wa Kiswahili. Kozi hizo na mihula yake imeelezwa katika sehemu inayofuata.

## 3.0 Kozi za Kusoma na Kuandika Kiswahili katika Idara

### 3.1 Madhumuni ya Jumla ya Kusoma

Madhumuni ya jumla ya kusoma na kuandika ni kumwezesha mwanafunzi kujua abjadi ya Kiswahili kwa jumla na kusoma na kuandika herufi zake kwa

hati ya Kirumi kwa umahiri. Aidha, kila muhula una malengo yake. Hapa chini kuna uchanganuzi wa malengo ya kila muhula katika kila kozi zinazohusika.

### 3.1.1 Madhumuni ya kila muhula

(a) Muhula wa Kwanza
Katika Muhula huu Kozi inayofundishwa ni
*SW 104: Kusoma na Kuandika*
Malengo yaliobainishwa ni: Mwanafunzi aweze kujua abjadi ya Kiswahili kwa jumla na kuandika herufi zake kwa hati ya kirumi kwa unadhifu.

(b) Muhula wa pili
Katika muhula huu wa pili kozi inayofundishwa ni SW 204: Kusoma na Kuandika; malengo hapa ni:
Mwanafunzi aweze kukamilisha ujuzi wake wa kusoma na kuandika maneno ya Kiswahili yenye herufi H-Z.

(c) Muhula wa Tatu
Katika muhula huu pia kuna kozi ya kusoma na kuandika, yaani
*SW 304: Kusoma na Kuandika*
Malengo ya kozi hii ni: Mwanafunzi aweze kutumia msaada atakaokuwa amepewa kukamilisha kazi anayotakiwa kutunga.

(d) Muhula wa Nne *SW 404: Kusoma na Kuandika*
Katika muhula huu kozi inayofundishwa ni SW 404: kusoma na kuandika. Malengo ya kozi hii ni:
Mwanafunzi akuze tabia ya kusoma na kuandika na kuweka kumbukumbu ya yale anayosoma na kuandika.
Kwa ujumla haya ndiyo madhumuni ya malengo ya kukuza stadi ya kusoma na kuandika yaliyobanishwa katika kozi zinazofundishwa idarani.

### 3.2 Mada za kusoma za kila muhula

Katika sehemu hii mada mbalimbali zinazolenga kukuza ujuzi wa kusoma zimebainishwa. Halikadhalka, mada hizo zimeorodheshwa kwa kuzingatia muhula, kozi na saa kwa wiki zinazotumika kufundisha.

(a) Muhula wa Kwanza
*SW 104: Kusoma na Kuandika*
Saa kwa wiki: 4
Mada zilizofundishwa:

1. Kusoma herufi zote za Abjadi ya Kiswahili (herufi A-Z )
2. Kusoma kwa makini na kuzingatia

(i) Herufi A-G
(ii) Silabi zinazoundwa kwa herufi A-G
(iii) Maneno yanayoundwa kwa herufi A-G

3. Kuandika kwa unadhifu:
   (i) Herufi ndogo na herufi kubwa A-G
   (ii) Silabi zinazoundwa kwa herufi A-G
   (iii) Maneno yanayoundwa kwa herufi A-G

4. Imla Uandikaji wa sentensi fupifupi zinazozingatia herufi, silabi na maneno yanayotokana na herufi A-G
5. Kusoma na Kuandika tarakimu 1-100 kwa maneno.

(b) Muhula wa pili

*SW 204: Kusoma na Kuandika*

Saa kwa wiki: 4

Mada za zilizopangwa kufundishwa:

1. Kusoma kwa makini na kuzingatia:
   (i) Herufi H-Z
   (ii) Silabi zinazotokana na herufi H-Z
   (iii) Maneno yanayotokana na herufi H-Z
   (iv) Majina ya siku za wiki na miezi

2. Kuandika kwa unadhifu:
   (i) Herufi ndogo na herufi kubwa H-Z
   (ii) Silabi zinazotokana na herufi H-Z
   (iii) Maneno yanayotokana na herufi H-Z
   (iv) Majina ya siku za wiki na miezi

3. Kuandika sentensi kwa njia ya imla kwa kutumia maneno yanayotokana na herufi zote A-Z
4. Kusoma na Kuandika tarakimu 1- 1000.

(c) Muhula wa Tatu

*SW 304: Kusoma na Kuandika*

Saa kwa wiki: 2

Mada zilizopangwa kufundisha:

1. Ujenzi wa msamiati kwa kusoma vitavuu vya mada mbalimbali k.m kilimo, ufundi, hadithi, ukoo wa familia yake, historia ya kabila n.k.
2. Kuimarisha kasi/wepesiwa kusoma na kuandika kwa:
   (i) kusoma vitabu kwa zamu darasani

(ii) Kuandika habari au matini kutoka kitabuni, kwa muda maalumu aliowekewa

(iii) Kuandika matini kwa njia ya imla

3. Kuandika hadithi /habari na kuisoma darasani
4. Kusoma na Kuandika tarakimu 1000 – 100.000 na pia namba zilizo katika vipimo
   Mbalimbali k.m 21%, 6.05, 1/3, 5/8 n.k .

(d) Muhula wa Nne
*SW 404*: *Kusoma na Kuandika*
Saa kwa wiki: 2
Mada zilizopangwa kufundishwa:
1. Ujenzi wa msamiati kutokana na:
   (i) Kusoma vitabu vya hadithi fupi na ndefu
   (ii) Magazeti au majarida

2. Kusoma vitabu au hadithi zilizo katika mfululizo fulani k.m. mchapishaji au mwandishaji mmoja

3. Kuandika hadithi kwa ajili ya kuchapisha katika gazeti la darasa, chama cha Kiswahili n.k

4. Kusoma vitabu vya idadi iliyowekwa na kutoa ripoti kwa kila kitabu kuhusu:
   (i) Muhtasari wa kitabu kilichosomwa
   (ii) Msamiati, semi au sentensi zilizomvutia.

**3.3 Vifaa vya kufundishia**

Vifaa na mbinu za kufundishia kusoma na kuandika vimepangwa kulingana na viwango mbalimbali na kwa mujibu wa muhula unaohusika. Kwa upande wa kusoma vitabu na vifaa vinavyotumika katika muhula wa kwanza na wa pili vinalenga, kwa kadiri inavyowezekana, kumwezesha mwanafunzi kusoma irabu na silabi za herufi zinazofundishwa katika muhula huo. Hii inamsaidia kukuza ujuzi anaoupata katika kusoma ili autumie baadaye katika kuandika. Ufundishaji wa Irabu si tatizo kubwa kwa sababu ni rahisi kutamka irabu. Ufundishaji wa konsonanti ni tofauti kwa sababu si rahisi kutamka konsonanti hasa inapokuwa haifuatwi na irabu.

Kwa mfano, ni vigumu kusoma konsonanti **b** peke yake kuliko kuisoma inapokuwa silabi **ba**. Hivyo ufundishaji wa konsonanti hufanywa kwa

kufundisha kusoma silabi zaidi - yaani konsonanti na irabu pamoja tangu mwanzo. Kwa Muhula wa Kwanza vitabu vyenye masomo ya irabu na silabi ndivyo vinavyotumika zaidi. Vitabu vingi kati ya hivi pia hufaa kwa kufundishia muhula wa pili ambapo konsonanti zaidi hufundishwa na pia kiwango cha kusoma neno zina huwa kimeanza. Vitabu vifuatavyo vinatumika kufundishia katika kiwango hiki:

1. *Kiswahili; Kusoma na Kuandika: Hatua ya Kwanza*
2. *Kitabu cha Kufundisha Kusoma na Kuandika (Darasa la Kwanza)*
3. *Kusoma: Kitabu cha 1* na *Kitabu cha 2*

Mbali na kuelekeza hatua za kusoma herufi, silabi na maneno, vitabu hivi pia vinaelekeza kuandika herufi mojamoja, hasa konsonanti. Ili kumsaidia mwalimu kuzingatia zaidi kufundisha herufi zilizopangwa kwenye muhtasari kadi maalumu za kusoma hutumika. Kadi hizi ziko katika viwango vitatu – yaani kadi za kusoma Irabu na Irabu na konsonanti (yaani silabi), kadi za kusoma maneno na kadi za kusoma sentensi fupifupi. Katika kufundisha silabi na neno, vitabu vyenye picha za vitu halisi na hasa picha zilichorwa kwa rangi vinasaidia zaidi. Mbali na kujua kusoma herufi, silabi au neno, mwanafunzi anaongeza pia msamiati wake. Hii ndiyo sababu vitabu vya Kiswahili kwa Walibya na pia Tuanze Kusoma vinasaidia sana kufundisha kusoma katika mazingira yetu.

### 3.4 Mbinu au Njia za Kufundishia Kusoma na Kuandika

Madhumuni ya jumla ya kufundisha kusoma na kuandika kama ilivyotajwa hapo juu ni kuwapa wanafunzi uwezo wa kumudu kusoma na kuandika Kiswahili. Hii ni kwa sababu lugha ambayo wanafunzi wanaitumia, Kiarabu, inatofautiana sana na Kiswahili kimaandishi (uundaji wa herufi, silabi na maneno). Hii huwalazimu walimu wa Kiswahili kufundisha hatua kwa hatua kuandika na kusoma lugha hii. Sehemu zifuatazo zinatoa ufafanuzi wa hatua hizo.

#### 3.4.1 Kufundisha Kusoma

Kwa kuwa stadi za kusoma na kuandika zinahusiana sana, irabu zote 5 zinafundishwa kwanza kabla ya konsonanti kufundishwa. Baadaye kila konsonanti inapofundishwa inabidi isomwe kwanza kwa kutamkwa na irabu /e/ ili iweze kutamwa kwa urahisi. Kwa mfano, konsonanti /**b**/ wakati wa kufundishwa inatamkwa kama [**be**] konsonanti, /**k**/ itamkwe kama [**ke**] wakati wa kufundishwa, /**j**/ kama [**je**] nakadhalika.

Baada ya kuibainisha konsonanti kama herufi, kila konsonanti inapofundishwa inaunganishwa na kila irabu ili kuunda silabi. Mfano, katika kujifunza kusoma

konsonanti /**b**/ kwanza itabainishwa kwa kusomwa kama [**be**]. Katika hatua inayofuata itasomwa pamoja na irabu zote tano na kuunda silabi $**ba**$ $**be**$ $**bi**$ $**bo**$ $**bu**$. Kadiri konsonanti zingine zitakavyosomwa mazoezi ya kuchanganya na konsonanti (silabi) zilizotangulia yanatolewa kwa wingi katika kusoma. Katika hatua hii maneno mafupi yanayotokana na silabi za konsonanti mojamoja huchanganya na konsonanti nyingine zinazofundishwa baadaye.

Kwa mfano: Katika kujifunza kusoma konsonanti /**b**/ **baba**, **beba**, **bibi**, **babu**, **boi**, **bua**, n.k
Kwa kuchanganya na konsonanti /**d**/ baadaye: **bado**, **debe**, **dubu**, **dudu**, **dua**, **dede**, n.k. Katika hatua za baadaye, baada ya kujifunza konsonanti za kutosha, usomaji wa maneno na sentensi kamili hufuata.

### 3.4.2 Kufundisha Kuandika

Stadi ya kuandika konsonanti iliyofundishwa huanza mara baada ya kufanya mazoezi mengi ya kusoma, kwa kuisoma vitabuni au kwenye kadi za kusoma silabi na maneno, na kuridhika kwamba wanafunzi wamepata ujuzi wa kutosha wa kuisoma konsonanti inayohusika. Baada ya hapo ufundishaji wa kuiandika unafanywa hatua kwa hatua. Sehemu muhimu zinazounda konsonanti hiyo zinafundishwa hatua kwa hatua mpaka umbo lake kamili linapokuwa limekamilika. Mwalimu huwaonesha wanafunzi sehemu na umbo zima la konsonanti hiyo kwa kuifuatisha hewani na baadaye hufundisha kuiandika ubaoni. Wanafunzi hufanya mazoezi ya kuiandika mpaka wanapokuwa wamefaulu. Kuandika maneno na sentensi ni hatua inayofanywa baada ya kupata ujuzi wa kuandika konsonanti za kutosha.

### 3.4.3 Kusoma na Kuandika Herufi Ambatano na Herufi Kubwa

Herufi Mwambatano ni herufi zaidi ya moja ambazo hutamkwa kama sauti moja. Mfano wa herufi hizo ni: **ng'**, **th**, **dh**, **kw**, **ngw**, **chw**, **fy**, **nyw**, **sh**, nakadhalika. Herufi **hzi** hufundishwa baada ya kukamilisha kusoma na kuandika maneno ambayo hayana herufi hizo. Hii ni kwa sababu hatua hii inahitaji ustadi na umakini zaidi kwa upande wa wanafunzi ambao sasa wanakutana na sauti tofauti na ngeni kutoka zile zilizo katika Kiarabu. Aidha, kusoma na kuandika herufi Kubwa kunafanywa kama hatua ya mwisho baada ya wanafunzi kupata ujuzi wa konsonanti za kawaida na konsonanti za mwambatano. Kulingana na muhtasari wa kufundishia kufikia muhula wa pili hatua hii inapaswa kuwa imefikiwa na kukamilika.

## 4.0 Changamano

Nchini Libya Kiswahili ni lugha ya kigeni kabisa. Wanafunzi wengi hawajawahi kuona maandishi yake wala kuisikia ikizungumzwa. Hivyo,

wanakutana nayo kwa mara ya kwanza kabisa wanapoingia muhula wa kwanza katika Idara ya Lugha na Taaluma za Kiafrika. Tofauti ya kwanza kubwa wanayoiona kati ya Kiswahili na Kiarabu ni kwamba Kiswahili kina sauti kadhaa ambazo hutamkwa tofauti, na nyingine hazimo kabisa katika Kiarabu. Kwa hakika kufundisha kusoma Kiswahili huanza na kufundisha utamkaji wa sauti za Kiswahili kuliko hata kufundisha kusoma kwenyewe.

Kwa upande wa kuandika, Kiswahili huandikwa kwa hati ya Kilatini ambayo ni tofauti kabisa na hati ya Kiarabu. Inabidi mwanafunzi ajifunze mambo mengi ya mtindo mpya kabisa wa kuandika. Humpasa ajue kuzifinyanga herufi za Kiswahili kwa hati ya Kilatini. Halikadhalika, inampasa awe makini kutofautisha kuandika herufi ndogo na herufi kubwa pamoja na kutii kanuni zote za uwakifishaji. Vilevile inambidi ajifunze na kuzoea kuandika kwa kuanzia kushoto kwenda kulia tofauti na alivyozoea anapoandika kwa Kiarabu. Katika muhula wa tatu na wa nne, anapofundishwa uandikaji bora inampasa ajue jinsi ya kuunganisha na kutenga maneno kwa usahihi kadiri ya silabi za Kiswahili. Kwa kawaida silabi nyingi za maneno ya Kiswahili zina muundo wa KI (Konsonanti na Irabu). Ni maneno machache sana yenye silabi zinazoishia na konsonanti. Katika Kiarabu silabi kuishia na konsonanti au neno kuwa na mkururo wa konsonanti ni muundo wa kawaida. Tofauti hizi ni changamoto kubwa kwa wanafunzi kuandika kwa usahihi maneno ya Kiswahili.

Changamoto nyingine inahusu vifaa vya kufundishia kusoma na kuandika. Vitabu vingi vinavyopatikana kwa urahisi vimeandiwa kwa wanafunzi ambao Kiswahili ama ni lugha yao ya kwanza au ni lugha ya pili na ambayo inazungumzwa katika mazingira wanamoishi. Hata vile ambavyo huonekana rahisi kwa wale ambao Kiswahili ni lugha yao vinahitaji marekebisho mengi ili viweze kuwafaa wanafunzi walio katika mazingira ya namna hii.

## 5.0 Mafanikio

Mbali na changamoto zilizotajwa ufundishaji wa Kusoma na Kuandika umekuwa na mafanikio makubwa katika idara. Hivi sasa muhtasari umechanganua kwa wazi zaidi mada zinazopaswa kufundishwa katika kila muhula kwa kupima ugeni wa lugha ya Kiswahili na wingi pamoja na uzito wa mada zinazoweza kufundishwa ndani ya kila muhula. Halikadhalika kuna maktaba ndogo ya vitabu vya Kiswahili na wanafunzi waanaweza kujisomea wanapokuwa nje ya darasa.

Vilevile kuna mkusanyiko wa kutosha wa vitabu vya Kiswahili katika maktaba ya ya Kitivo cha Sanaa. Mbali na vitabu vya maktaba vingi ambavyo vinatoka

Kenya na Tanzania, waandishi mbalimbali Walibya waliofuzu Kiswahili wameanza kujitokeza kuandika vitabu vinavyozingatia mazingira ya Libya kwa ajili ya wanafunzi kujifunza kusoma na kuandika Kiswahili katika viwango vya Sekondari na Chuo (tazama Viambatisho A na B).

## 6.0 Mapendekezo ili Kupata Mafanikio Zaidi

Mbinu zinazotumika kufundisha kusoma na kuandika kwa sasa zina mafanikio kwa kiwango fulani. Jambo linalotakiwa ni jinsi ya kupata mbinu nyingine zaidi ili kufanikisha ufundishaji kusoma na kuandika kwa haraka zaidi. Yafuatayo ni kati ya maeneo makuu ambayo yanaweza kufanyiwa utafiti ili kubuni mbinu bora zaidi:

### 6.1 Vitabu na vifaa vya kufundishia

Ni muhimu kujiuliza na kupata majibu kwa maswali yafuatayo kwa ajili ya kufanikisha ufundishaji wa stadi za kusoma na kuandika:

(1) Je, vitabu vilivyopo vina uzuri gani na hitilafu zipi ambazo zinapaswa kurekebishwa kwa ajili ya kufundishia kusoma na kuandika?

(2) Je, vifaa gani mbali na vitabu, vinatakiwa vitumike ili kufanikisha ufundishaji wa kusoma na kuandika? Mathalani: kadi za kusoma, picha, vitu halisi, chati n.k. na vifaa hivyo viwe na sifa gani?

### 6.2 Mbinu za kusoma na kuandika nje ya darasa

Kujifunza kusoma na kuandika kunapaswa kusikomee darasani tu bali pia mwanafunzi anapaswa kupata fursa za kutumia stadi hizo nje ya darasa. Hivyo mashindano ya aina mbalimbali yanapaswa kufanyika. Yafuatayo ni kati ya maswali ya kujiuliza kwa ajili ya mbinu hiyo:

(1) Je, ni aina gani ya mashindano ya kusoma yanafaa kwa ajili ya wanafunzi kwa kila kiwango?

(2) Je, mashindano ya kusoma yalenge kupata mafanikio yapi kuhusu: ufasaha wa kutamka, kasi ya kusoma, ustadi wa kusoma?

(3) Je, ni aina gani ya mashindano yanafaa kwa ajili ya kukuza uandikaji wa wanafunzi kwa kila kiwango?

(4) Je, mashindano ya kuandika yalenge kupata mafanikio yapi? Mfano, kuepuka makosa ya kitahajia, unadhifu wa mwandiko, n.k.

## 7.0 Hitimisho

Katika makala haya tumeona ya kwamba katika ulimwengu wa leo, mwanafunzi anayejifunza lugha, hasa lugha ya Kigeni, kujua kuizungumza lugha peke yake hakutoshi. Kwa sababu ya mahitaji mbalimbali ya kurahisisha

mawasiliano baina yake na wasemaji wa lugha hiyo na pia kwa mahitaji ya kujua zaidi mambo ya kale na ya sasa yaliyohifadhiwa katika lugha hiyo, inampasa mwanafunzi huyo ajue pia kuisoma na kuiandika lugha hiyo ili uhitimu wake uweze kukamilika. Tumeona pia kwamba kujifunza kusoma na kuandika lugha ya kigeni kuna matatizo mengi. Miongoni mwa hayo ni kujua mfumo wa lugha ngeni yaani sauti zake na jinsi zinavyowakilishwa katika maandishi, muundo wa silabi, maneno na hata sentensi zake. Lakini mafanikio hupatikana iwapo mwanafunzi atazingatia kwa makini hatua madhubuti ambazo lazima azipitie ili kupunguza matatizo wakati wa kujifunza na pia ili kufikia kiwango kinachotakiwa cha ustadi wa kusoma na kuandika. Ubunifu wa mwalimu kuhusu mbinu za kumsaidia mwanafunzi na pia vifaa vya kumwezesha kusoma au kuandika kwa usahihi ni mambo ambayo lazima yatiliwe mkazo tangu mwanzo. Kama msingi huu ukiwa imara uandikaji na usomaji wa mwanafunzi wa baadaye utaendelea kuimarishwa kwa urahisi.

## Marejeo

Idriss, H. E. (2009). *Tuanze Kusoma.* Sebha, Libya: Sebha University

Mkuki na Nyota (1993). *Karibu tusome Kiswahili.* Dar es Salaam

Oxford University Press. (2006). *Kiswahili 1 Shule za Msingi* Toleo la Pili. Dar es Salaam.

__________ (2006). *Kiswahili 2 Shule za Msingi.* Dar es Salaam.

__________ (2006). *Kiswahili 3 Shule za Msingi.* Dar es Salaam.

Rafiki Publishers. (2006). *Kiswahili Kusoma na Kuandika. Hatua ya kwanza.* Zanzibar

Taasisi ya Elimu Tanzania. (2005). *Kitabu cha Kufundisha Kusoma na Kuandika (Darasa la Kwanza)* Toleo la 6. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House

__________ (2005). *Kusoma: Kitabu cha 1 (Darasa la Kwanza)* Toleo la 7. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House

__________ (2005). *Kusoma: Kitabu cha 2 (Darasa la Kwanza)* Toleo la7. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House

__________ (2005). *Kusoma: Kitabu cha 3 (Darasa la Pili)* Toleo la 7. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House

__________ (2005). *Kusoma: Kitabu cha 4 (Darasa la Pili)* Toleo la 7. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House

## KIAMBATISHO A

## VITABU VILIVYOTUNGWA NA WANATAALUMA NCHINI LIBYA KWA AJILI YA KUFUNDISHA KISWAHILI KATIKA SHULE ZA SEKONDARI, LIBYA

| | |
|---|---|
| *Kiswahili Sekondari I –* | ***Mazungumzo*** Idara ya Mitaala Kamati ya Elimu Libya, 2007 |
| *Kiswahili Sekondari I –* | ***Sarufi*** Idara ya Mitaala Kamati ya Elimu Libya, 2007. |
| *Kiswahili Sekondari I* | ***Ufahamu*** Idara ya Mitaala Kamati ya Elimu Libya, 2007. |
| *Kiswahili Sekondari I* | ***Kusoma na Kuandika*** Idara ya Mitaala Kamati ya Elimu Libya 2007. |
| *Kiswahili Sekondari I* | ***Matamshi*** Idara ya Mitaala Kamati ya Elimu Libya 2007. |
| *Kiswahili Sekondari I* | ***Maabara ya Lugha*** Idara ya Mitaala Kamati ya Elimu Libya 2007. |
| Kiswahili kwa Walibya | ***Kitabu cha Mwanafunzi II*** Idara ya Mitaala Kamati ya Elimu Libya 2008. |
| Kiswahili kwa Walibya | ***Kitabu cha Mazoezi II*** Idara ya Mitaala Kamati ya Elimu Libya 2008. |
| Kiswahili kwa Walibya | ***Kitabu cha Mwalimu II*** Idara ya Mitaala Kamati ya Elimu Libya 2008. |
| Kiswahili kwa Walibya | *Kiswahili kwa Walibya* ***Kitabu cha Mwanafunzi III*** Idara ya Mitaala Kamati ya Elimu Libya 2009. |
| Kiswahili kwa Walibya | *Kiswahili kwa Walibya* ***Kitabu cha Mazoezi III*** Idara ya Mitaala Kamati ya Elimu Libya 2009. |
| Kiswahili kwa Walibya | *Kiswahili kwa Walibya* ***Kitabu cha Mwalimu III*** Idara ya Mitaala Kamati ya Elimu Libya 2009. |